



Somo nilipendalo



Tusome Early Literacy Programme


Somo nilipendalo




Leo asubuhi mwalimu wetu Nekesa ametuita sote pamoja. Watoto wote wa darasa la kwanza wanapangwa katika vikundi vitatu. Kila kikundi kina wasichana na wavulana.

Mwalimu Nekesa anataka watoto wasome somo la sayansi. Kikundi cha kwanza kimepewa jina Siafu, cha pili Nyigu na cha tatu Nyuki. Kila kikundi kinachagua kiongozi.





Mwalimu Nekesa anataka kila kikundi kilete vitu tofauti tofauti. Siafu wataleta ndizi tano na Nyigu walete ndimu kumi. Nyuki nao walete mapera sita.




Mwalimu amewapa dakika thelathini kufanya kazi hiyo. Kila kiongozi anaongea na kikundi chake. Vikundi vyote vinaachana na kwenda uwanjani.

Siafu wanatimua mbio kutafuta ndizi. Wanamwona mfanyikazi wa shule na kumuomba awapatie ndizi tano. Anakubali na kuwapatia.



Nyigu pia wanakimbia kuelekea shambani. Kiongozi anaupanda mdimu na kuchuma ndimu kumi ndogo. Wote wanarudi darasani.






Nyuki wanajua mpera mmoja tu shuleni.
Wanakimbia huko na kupata mapera sita yaliyoiva.
Wanampelekea mwalimu Nekesa.

Watoto wote wamezunguka meza ya mwalimu. Mwalimu Nekesa anachukua ndimu tisa, ndizi tano, mapera matano na kuyakata. Anapatia kila kikundi vipande vya ndimu, ndizi na mapera.






Mwalimu anawauliza wanachokiona ndani ya kila kipande. Watoto wanainua mikono. Wanataja vitu mbalimbali.

Mwalimu Nekesa
anawaambia kuwa kila
tunda huwa na mbegu.
Wanaangalia ndizi na
kushangaa. Mwalimu
anawaonyesha mbegu
ndogo za ndizi.



Kisha, mwalimu Nekesa anawaambia wachore kila tunda lote. Halafu wachore vipande vya kila tunda. Mwishowe, waandike majina chini ya kila picha.





Mwalimu Nekesa anawachorea mifano katika ubao.
Watoto wote wanachora na kuandika majina.
Watoto wote wanafurahia somo la Sayansi.

Maswali

1. Watoto wanapangwa katika vikundi vingapi? Taja majina ya vikundi hivyo.
2. Taja vitu ambavyo kila kikundi kiliagizwa kuleta.
3. Nyuki walileta mapera mangapi?
4. Mwalimu Nekesa alichukua matunda mangapi?
5. Unafikiri watoto waliona nini ndani ya vipande walivyopewa na Mwalimu Nekesa?

Somo nilipendalo

Mwalimu Nekesa ana mbinu mpya ya kufunza wanafunzi somo la hesabu. Wanafunzi wanatakiwa wakusanye matunda tofauti kwa vikundi. Je, mwalimu Nekesa atayatumia vipi matunda hayo katika somo?



Kitabu hiki kimechapishwa kwa ufadhili kutoka kwa Shirika la maendeleo ya kimataifa la Marekani (USAID/Kenya) na Idara ya maendeleo ya kimataifa ya Uingereza (DFID/Kenya) kupitia mradi wa Tusome Early Grade Reading Activity.